

Maana ya ‘taabu haitoki mchangani, Wala mashaka hayachipuki katika nchi’ ni nini?

Ayubu 5:6 “Kwani taabu haitoki mchangani, Wala mashaka hayachipuki katika nchi;”

Watu wengi tumekuwa tukilaumu mazingira, tukilaumu wanyama, tukilaumu ardhi, na vitu vingine vya asili kuwa ndio chanzo cha matatizo yetu, chanzo ya shida zetu na mashaka yetu rohoni. Lakini maandiko yanatupa uhalisia kwamba taabu na mashaka havichupuki ardhini, kama vile mchicha umeavyo, bali vinatoka ndani yetu wenywewe.

Makosa yetu ndio zao la kila aina ya matatizo yetu. Asili ya migogoro katika ndoa, sio ule m-buyu uliokaribu na nyumba zetu. Unaweza kuhama hata nchi ukakaa chini ya mizeituni na mizabibu mizuri, na maua, lakini bado ndoa yako ikaendelea kuwa na matatizo tena makubwa zaidi hata yale ya mwanzo.

Sababu ya kuteswa na mapepo, sio Yule paka mweusi wa jirani anayekuja kulala batini kwako kila siku usiku. Bali ni kwasababu Kristo hayupo ndani yako.

Sababu ya kutokupiga hatua kiroho, sio hiyo ardhi unayoishi, au

Maana ya ‘taabu haitoki mchangani, Wala mashaka hayachipuki
katika nchi’ ni nini?

unayoimiliki, usihangaike na maombi ya kufungua/ kukomboa ardhi,
hangaike na vifungo vilivyomo ndani yako. Ambavyo vinatokana na
aidha kutolielewa Neno la Mungu, au kuwa nje ya wokovu.

Biblia inasema..

*Yohana 8:36 Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli
kweli.*

Na tena inasema...

*Yohana 8:32 “tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka
huru”.*

Rekebisha mwenendo wako, pokea wokovu wa kweli, kisha liishi Neno la Kristo kila siku. Hakika utaona jinsi tatizo lako linavyotalika kirahisi, ndipo utaacha kuyalaumu mazingira ya nje.

Ayubu 5:6 “Kwani taabu haitoki mchangani, Wala mashaka hayachipuki

Maana ya 'taabu haitoki mchangani, Wala mashaka hayachipuki
katika nchi' ni nini?

katika nchi;"

Je! Umeokoka? Kama bado unashubiri nini? Je! Unatambua kuwa hizi ni siku za mwisho, na Kristo yupo mlangoni kurudi, tunaishi katika muda wa nyongeza tu, siku yoyote unyakuo wa kanisa unapita, watakatifu kuchukuliwa mbinguni na wenyewe dhambi kwenda motoni?. Fanya uamuzi sahihi sasa, ikiwa upo tayari kuokoka leo, basi fungua hapa kwa mwongozo huo >>> **KUONGOZWA SALA YA TOBA**

Bwana akubariki.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Mada Nyinginezo:

MTU MWENYE KUSITA-SITA KATIKA MAWAZO MAWILI.

LAKINI WAKATI WA TAABU WATASEMA, SIMAMA UKATUOKOE.

Maana ya 'taabu haitoki mchangani, Wala mashaka hayachipuki
katika nchi' ni nini?

Rafiki hupenda sikuzote; Na ndugu amezaliwa kwa siku ya taabu.

VITABU VYA BIBLIA: Sehemu ya 9 (Kitabu cha Ayubu).

Uasherati wa Kiroho maana yake nini?

Rudi nyumbani

Share on:

WhatsApp